JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI
WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI

Ofisi ya Meneja RUWASA Wilaya ya Wanging'ombe, S.L.P 141, Njombe
wangingombedm@ruwasa.go.tz

Tarehe: 22.04.2022

MHE. MWENYEKITI,
BARAZA LA MADIWANI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU (JANUARI – MACHI) MWAKA 2021/2022

1.0 UTANGULIZI

Mhe. Mwenyekiti,
Katika kipindi cha Januari - Machi 2021/2022, Wakala ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini wilaya ya Wanging'ombe (RUWASA) imeendelea na utekelezaji wa miradi ya maji 5 kama ilivyoainishwa kwenye *Jedwali A* la taarifa hii.

2.0 TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KWA BAJETI YA MWAKA 2021/2022

Mhe. Mwenyekiti,
Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilaya ya Wanging'ombe iliidhinishiwa kiasi cha shilingi **2,550,134,152.00** kutoka vyanzo mbalimbali; Shilingi **1,416,052,968.00** kutokana na programu ya malipo kwa matokeo (PbR), shilingi **803,678,024.00** kutoka mfuko wa maji wa Taifa (NWF) na shilingi **330,403,160.00** kutoka Serikali kuu.

Mhe. Mwenyekiti,
Katika kipindi cha Januari – Machi 2021/2022 Ofisi ilipokea taarifa ya mapokezi ya kiasi cha shilingi **354,013,242.00** katika akaunti ya RUWASA Mkoa kutoka fedha za malipo kwa matokeo (PbR) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji robo ya tatu. Fedha hizo zilielekezwa kugawanywa katika mchanganuo ufuatao;-

• Ujenzi wa miundombinu (70%)	= 247,809,269.40
• Maandalizi ya miradi (6%)	= 21,240,794.52
• Usimamizi wa miradi na uendeshaji wa ofisi (10%)	= 35,401,324.20
• Ukaguzi (2%)	= 7,080,264.84
• Uendelevu wa miradi (12%)	= 42,481,589.08
Jumla	354,013,242.00

Aidha, kiasi cha shilingi **881,930,678.40** kilipokelewa ikiwa ni fedha kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi **M/S STC JV YELL Ltd.** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji kwa vijiji vya Malangali na Hanjawanu (Igando - Kijombe).

3.0 UTEKELEZAJI WA MRADI KWA FEDHA ZA COVID - 19

Mhe. Mwenyekiti,

Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira vijijini (RUWASA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini (WANGIWASA) inatekeleza mradi wa uboreshaji wa upatikanaji wa maji katika mradi wa maji wa kitaifa wa Wanging'ombe - kijiji cha Igula kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19. Jumla ya **shilingi 456,200,100.00** zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji huo, na katika kipindi cha Januari - Machi 2021/2022, shilingi **270,871,816.00** zilipokelewa.

Mhe. Mwenyekiti,

Naomba kuwasilisha,

Eng. Charles M. Mengo
MENEJA WA RUWASA
WILAYA YA WANGING'OMBE

JEDWALI A: MIRADI INAYOENDELEA NA UTEKELEZAJI

Na.	JINA LA MRADI	MKANDARASI	GHARAMA YA MRADI (TSH.)	MALIPO YALIYOFANYIKA (TSH)	HATUA YA UTEKELEZAJI	Maelezo
1.	Ujenzi wa mradi wa maji mtiririko vijiji vya Malangali na Hanjawanu (Igando - Kijombe)	M/S STC JV YELL LTD. P.o.Box 4440, DAR ES SALAAM.	12,437,407,360.00	4,857,354,462.16	• Ujenzi wa mtego wa maji (95%), • Ujenzi wa bomba kuu km. 28.94 (43.5%) • Ujenzi wa chujio (92%) • Ujenzi wa Tenki la kuhifadhia maji lita 100,000 (90%) • Ujenzi wa Tenki la kuhifadhia maji lita 100,000 kwenye mnara wa m.9 (97%) • Ujenzi wa bomba la kusambaza maji km. 18.238 (80%) • Ujenzi wa vituo vya kuchotea maji 22 (100%) • Ujenzi wa miundombinu ya kunywea maji mifugo 2 (99%) • Kutoa mafunzo ya uendeshaji wa skimu kwa watu 2 (50%)	Mkandarasi anaendelea na Ulazaji wa Bomba kuu, kuunganisha vituo vya Hanjawanu na kukamilisha kazi ambazo ziko hatua za mwisho *(zilizotekelezwa zaidi ya 90)* Changamoto; *Kujaa kwa mchanga na mmomonyoko wa udongo eneo la mtego wa maji (Intake) kutokana na maporomoko ya maji kipindi cha mvua*

Na.	JINA LA MRADI	MKANDARASI	GHARAMA YA MRADI (TSH.)	MALIPO YALIYOFANYIKA (TSH)	HATUA YA UTEKELEZAJI	Maelezo
2.	Uboreshaji wa upatikanaji wa maji kwa mradi wa maji wa Kitaifa Wanging'ombe	FORCE ACCOUNT	456,200,100.00	71,593,821.57	• Ujenzi wa Tenki lita 150,000 kwenye mnara wa m.12 (70%) • Ujenzi wa nyumba ya mtambo wa kusukuma maji (80%) • Ujenzi wa bomba kuu km. 1.95 na Ujenzi wa bomba la kusambaza maji km. 7.6 (90%) • Ujenzi wa vituo vya kuchotea maji 5 (60%)	Mradi unaendelea na utekelezaji
3.	Upanuzi wa miradi ya maji mtiririko katika vijiji vya Kinenulo, Imalilo, Masaulwa, Moronga (Kilanzi)	M/S MWANSHINGA ENTERPRISES Co. LTD, P.O. Box 855, Dodoma	516,898,959.62	0.00	Mkandarasi alikabidhiwa eneo la mradi Tarehe 19.04.2022.	Kwa mujibu wa Mkataba, ujenzi utaanza ndani ya siku 7 baada ya makabidhiano ya eneo la mradi
4.	Upanuzi wa mradi wa maji mtiririko katika kijiji cha Wangamiko na Mpanga	-	3,760,900,034.56	-	Taarifa ziliwasilishwa ofisi ya Mencja wa Mkoa kwa ajili ya kutangaza zabuni	Utekelezaji utaanza mara baada ya kupata Mkandarasi

Na.	JINA LA MRADI	MKANDARASI	GHARAMA YA MRADI (TSH.)	MALIPO YALIYOFANYIKA (TSH)	HATUA YA UTEKELEZAJI	Maelezo
5.	Upanuzi wa mradi wa maji mtiririko Ng'anda - Uhekule	FORCE ACCOUNT	517,972,843.18	-	• Usanifu na maandalizi ya mahitaji ya vifaa vimekamilika. • Taratibu za ununuzi kupata Fundi na Vifaa vya Ujenzi zinaendelea	Muda wa kuanza utekelezaji ulisogezwa hadi Mwezi Mei, 2022 kutokana na eneo la chanzo kutofikika wakati wa mvua nyingi.

****

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA TANESCO NA REA KWA MWAKA WA FEDHA KUANZIA

JULY 2021 – SEPTEMBER 2022 21.04.2022

Mheshimiwa mwenyekiti

Wilaya yetu ya Wanging'ombe kwa mwaka wa fedha wa 2021 – 2022 ilipata miradi kumi na tatu (13) ambayo inatekelezwa na Tanesco nayo ni :

- Igwachanya kati Tshs. 21,625,678.97
- St. Monica Secondary Luduga Tshs. 56,231,943.69
- Dr. Dugange Secondary ItulahumbaTshs.4,840,271.81
- Igwachanya CCM Tshs. 5,593,096.38
- Ilembula Hospital Tshs. 14,581,375.34
- Ilembula Kiginga Tshs. 26,500,988.04
- Ilembula Luwande Tshs. 26,499,726.25
- Luduga Tshs. 9,958,10.24
- Mdandu Msindo Tshs. 14,012,957.02
- Elly English medium Primary schoolTshs.5,789,878.85 Miradi hii imekamilika
- Kiduala mkeha Tshs. 33,501,203.00

Mradi ambayo haija kamilika

- Chalowe Tshs. 44,828,902.00
- Makoga Mgoda Tshs. 17,791,943.00

Miradi inayotekelezwa na Rea Three Roumnd two kwa mwaka wa fedha wa July 2021 – June 2022 Wilaya ya Wanging'ombe imebahatika kupata vijiji nane (8) ambavyo ni:

1. Hanjawanu
2. Mpanga
3. Malangali
4. Masaulwa
5. Imalilo
6. Idunda
7. Wangamiko
8. Nyumbanitu

Vijiji hivi vyote vimeshafanyiwa Survey na mkandarasi amesha peleka nguzo kwenye vijiji sita (6) ambavyo bado ni viwili (2) wangamiko na nyumbanitu mkandalasi huyo anaitwa SILO POWER.

CHANGAMOTO

1. Matengenezo yanayoendelea kwenye vituo vya kupoozea umeme yanasababisha kukatika kwa umeme
2. Kukatika kwa umeme kutokana na wananchi kuchoma moto nguzo

.....

Ag. DISTRICT MANAGER – WANGING'OMBE

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WAKALA WA BARABARA ZA VIJIJINI NA MIJINI-TANZANIA (TARURA)

TANZANIA RURAL AND URBAN ROADS AGENCY
TARURA
Improved Roads For Sustainable Development

S.L.P 840,

WANGING'OMBE-NJOMBE

22/04/2022

YAH: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA BARABARA NA MADARAJA KWA MWAKA FEDHA 2021/2022

1. **Utangulizi**
   Mhe: Mwenyekiti

Wakala wa barabara za Mijini na Vijijini Wilaya ya Wanging'ombe (TARURA) ina mtandao wa barabara wenye jumla ya kilometa 1,040.65 ambao umehakikiwa,Katika barabara hizo TARURA Wilaya ya Wanging'ombe ina barabara za **Lami Km.6.9**, Barabara za **changarawe Km.171.66Km** na barabara za **Udongo Km.862.09** vilevile katika barabara hizo kuna **Madaraja 76** na **Makalvati 312**

2.0 Utekelezaji wa Matengenezo na Ujenzi wa Barabara na Madaraja.
Mhe: Mwenyekiti

Halmashauri ya Wilaya Wanging'ombe kwa mwaka wa fedha 2021/2022 iliingia mikataba na wakandarasi yenye kiasi cha **Tshs. 1,290,457,195.00** kwaajili ya matengenezo na Ujenzi wa Barabara Kilomita 109 na ujenzi wa vivuko vinne(4) kwa kulingana na bajeti iliyoidhinishwa.Pia katika mwaka 2021/2022 tunaendelea na utekelezaji wa ujenzi wa daraja la Saja – Idenyimembe **Tshs. 634,112,000.00** ambao ni mradi wa mwaka wa fedha

2020/2021.Kwahivi sasa miradi hiyo imekamilika kwa **90.3%** kazi utekelezaji wake upo katika **kiambatanisho A**

2.1 Utekelezaji wa miradi ya TOZO za mafuta
Mhe: Mwenyekiti
Halmashauri ya Wilaya Wanging'ombe kwa mwaka wa fedha 2021/2022 iliingia mikataba na wakandarasi yenye kiasi cha **Tshs. 1,932,000,000.00** kwaajili ya Ujenzi wa Barabara Kilomita 77.08 kwa kiwango cha changarawe kutokana na fedha za Tozo za mafuta utekelezaji wa miradi umefikia asilimia 38 na kazi zinaendelea.Utekelezaji wake umeonyeshwa katika **kiambatanisho B.**

2.1 Utekelezaji wa mradi wa JIMBO
Mhe: Mwenyekiti
Halmashauri ya Wilaya Wanging'ombe kwa mwaka wa fedha 2021/2022 iliingia mkataba na Mkandarasi M/s Pripam Co.LTD wenye kiasi cha **Tshs. 498,572,000.00** kwaajili ya Ujenzi wa lami Kilomita 1 na taa za barabarani 16 kutokana na fedha za Tozo za miamala ya simu.Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 90 na kazi zinaendelea.Utekelezaji wake umeonyeshwa katika **kiambatanisho B.**

3.0 Changamoto
Mhe: Mwenyekiti
Kwa ujumla kuna changamoto nyingi ambazo Wakala inakabiliana nazo katika kupanga na kutekeleza mipango mbalimbali inayohusu mindombinu ya barabara. Pamoja na wingi wa changamoto hizo, zifuatao ni changamoto kubwa:-

a) Hali ya hewa ya mvua ambayo husababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi kwa wakati
b) Ufinyu wa bajeti kulingana na mtandao wa barabara.
c) Upitishaji wa mifugo barabarani unaopelekea uharibifu mkubwa wa barabara.
d) Uzibaji wa mitaro ya kutoa maji katika barabara

e) Ujenzi na shughuli za kilimo katika hifadhi ya barabara
f) Uzidishaji wa uzito wa magari katika barabara zetu.
g) Upatikanaji wa changarawe nzuri na ikipatikana tunalazimika kuinunua kwa gharama kubwa inayopelekea kupunguza ukubwa wa utekelezji wa kazi.

7.0 JITIHADI TULIZOZIFANYA KATIKA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

Mhe: Mwenyekiti

a) Kuhakikisha kuwa kazi za barabara zinatangazwa mapema mara baada ya kupitishwa bajeti na kukamilisha taratibu nyingine za kisheria
b) Tumeendelea kuandaa maandiko mbalimbali kwaajili ya kuomba miradi pia tumeendelea kuomba TARURA Makao makuu watuongezee bajeti hii ni kulingana na mtandao wetu wa barabara.
c) Tumeanza kuandaa vipeperushi pamoja na elimu kwa watendaji na Waheshimiwa Madiwani ili waweze kutufikishia kwa wananchi juu matumizi sahihi ya barabara
d) Katika bajeti hii na zijazo tutaandaa alama katika baadhi ya barabara ya kuonyesha hifadhi ya barabara.
e) Tutaendelea kutoa elimu juu ya athali za uzidishaji wa mizigo pia *tumeendelea kuomba kupewa mizani*

Nawasilisha

Eng.Boniface Kasambo
Meneja wa TARURA
Wilaya ya Wanging'ombe

KIAMBATANISHO "A"

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA BARABARA NA MADARAJA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Na.	Jina la Mradi	Mkandarasi	Gharama ya Mradi	Fedha iliyotumika	Tarehe ya kuanza	Tarehe ya kumaliza	Hatua iliyofikia hadi sasa (%)	Maelezo /Changamoto
1	Matengenezo ya Muda Maalumu barabara za Usalule-Lugenge 4km, Ujindile-Igodivaha 1km, Usalule-Lugenge 2km, Kipengele-Lupila 1.5km,Igima-Mdandu 1.3km, Matengenezo ya sehemu korofi barabara za Ujindile-Igodivaha 4.3km, Idunda-Ivigo-Igosi 3km, Usalule-Lugenge 4.4km, Igima-Mdandu 3.5km,Nyumbanitu-Estate No.5 4km Matengenezo ya kawaida barabara ya Ulembwe-Madasi 4.3Km	MS ROTY COMPANY LIMITED, S.L.P 1251, IRINGA	284,049,751.00	136,852,500.00	21/08/2021	02/05/2022	64%	Kazi zinaendelea
2	Matengenezo ya kawaida barabara ya Kidugala-Massage-Masilu 3.75km, Lugalo-Ilulu 2.46km, Malangali-Soliwaya 5km, Kidugala-Gonelamafuta 2km, Matengenezo ya sehemu korofi barabara za Malangali-Wangamiko 2.45km, Masaulwa-Itambo 3.26km, Mtapa-Kidugala-Masilu 4km, Estate No.5-Imalinyi-Kidugala 3.4km na Ujenzi wa daraja mkeka (Vented Drift) barabara ya Malangali Wangama.	MS VICIDAH INVERSTMENT CO LIMITED, S.L.P 3018, MBEYA	164,552,900.00	105,290,400.00	27/08/2021	02/05/2022	98.49%	Mkandarasi anaendelea na kazi ya kuweka kalvati
3	Matengenezo ya kawaida barabara ya Isimike-Igomba 1.8km, Kijombe-Ukomola 2km, Matengenezo ya sehemu korofi barabara za Saja-Makondo 1km, Ikwavila-Uhenga-Idofi 1.8km, Ikwavila-Kijombe 4.2km, Matengenezo ya daraja barabara ya Uhenga-Katenge,Matengenezo ya daraja la Saja-Makondo	MS GREENNAXIS CO LTD, S.L.P 36, MBEYA.	199,708,400.00	199,208,400.00	21/08/2021	21/02/2022	100%	Kazi zimekamilika bado marekebisho baadhi ya maeneo
4	Matengenezo ya kawaida barabara ya Mwilongo-Igombatavanga 3.94km,	RIDE		51,999,000.00				Mkandarasi

	Alfred National Housing 1.05km, Usuka-Udonja 3.67km, Matengenezo ya sehemu korofi barabara za Iteni-Usuka-Matowo 3km, Ihanzutwa-Sakalenga 3km, Lulanzi-Ibumila 3.01km Ujenzi wa daraja mkeka (Vented Drift) barabara ya Igwachanya Kati-Nmb-Igwachanya na matengenezo ya kalvati Ilembula-Wanging'ombe.	INVESTMENT CO LTD, S.L.P 886, IRINGA	88,450,350.00		27/08/2021	02/05/2022	78.78%	anaendelea na kazi ya kujenga kalvati barabara ya Ilembula-Wanging'ombe
5	Matengenezo ya daraja barabara ya Ilembula-Wangingombe, Ujenzi wa daraja mkeka (Vented Drift) barabara ya Uhambule-Ufwala, Ujenzi wa daraja mkeka (Vented Drift) barabara ya Itombololo-Chai	MS OSBORN COMPANY LTD, S.L.P 33845, DAR ES SALAAM	95,915,500.00	93,815,500	27/08/2021	27/02/2022	100%	Kazi zimekamilika
6	Matengenezo ya kawaida barabara za – Ufwala 3.83km, Ilembula – Kanamalenga 3.6km, Matengenezo ya sehemu korofi barabara za Banawanu – Ngamanga 4.4km, Utiga – Lyadebwe – Mayale 3km, Kasagala – Image 4.50km, Ilembula – Luduga 2.7km, Kanamalenga – Mpululu 4km Luduga – Malangali 4km Ujenzi wa daraja mkeka (Vented Drift) barabara ya Korinto – Luduga	MS FESA BUILDING AND CIVIL CONSTRUCTION CO.LTD, S.L.P 11, IRINGA	176,239,600.00	175,457,600.00	27/08/2021	27/02/2022	100%	Kazi zimekamilika
7	Ujenzi wa barabara ya Ihanja-Itambo-Imalinyi 13.6km kwa kuiwekea changarawe	MS GWEMA GENERAL ENTERPRISES, S.L.P 2016, IRINGA	426,658,000.00	194,736,000.00	21/08/2021	02/05/2022	95.85%	Mkandarasi anaendelea na kazi ya kuchimba mifereji ,kujenga mifereji na ujenzi wa makalvati
8	Ujenzi wa daraja katika barabara ya Saja-Idenyimembe	MS BERASI INVESTIMENT CO LTD, S.L.P 240, MBEYA	634,112,000.00	408,685,400.00	17/06/2021	3/02/2022	92.46%	Mkandarasi anaendelea kumwaga zege la deki ya daraja

KIAMBATANISHO B

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA BARABARA NA MADARAJA KWA FEDHA ZA JIMBO

1	Ujenzi wa barabara kiwango cha lami barabara za Ilembula Mjini (Barabara ya Ilembula Hospital -Ilembula Markert Road 0+000 - 0+070, Barabara ya Ilembula - Kanamalenga 0+400 - 1+080 ,Barabara ya Ilembula- Igelehedza 0+020 - 0+ 300	MS PRIPAM CO.LTD P.O.BOX 825, IRINGA.	456,572,600.00	222,518,500.00	21/09/2021	10/05/2022	90%	kazi zinaendelea.uwekaji wa taa pamoja na kujenga mifereji

KIAMBATANISHO B

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA BARABARA NA MADARAJA KWA FEDHA ZA TOZO YA MAFUTA

1	Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha Changarawe barabara za kata ya Wanging'ombe km 5, Ujenzi wa Barabara Kwa Kiwango Cha Changarawe Barabara za Mtapa—Mambegu –Kidugala km 14.4, Ilembula-Luduga Km 6,Estate No.5-Imalinyi Km 10 na Ujenzi Wa Drifti Katika Barabara ya Lugoda-Matipu.	MS GWEMA GENERAL ENTERPRISES, S.L.P 2016, IRINGA	*1,024,932,000.00*	337,735,000.00	13/1/2022	13/07/2022	65%	Mkandarasi anaendelea na kazi ya changarawe na makalvati

2	Ujenzi Wa Barabara Kwa Kiwango Cha Changarawe Barabara Za Igosi-Ujindile km 16.9 Kinenulo-Makoga 12.6 na Mafinga-Mwilamba Km 7	MS GWEMA GENERAL ENTERPRISES, S.L.P 2016, IRINGA	876,000,000.00	NIL	08/02/2022	08/08/2022	12%	Mkandarasi anaendelea na kazi ya kusafisha na kuchonga barabara Igosi-Ujindile-Wangama

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO KAZI 2021/2022 TFS WANGING'OMBE KWA KIPINDI CHA JULAI – MARCH 2022

A: UTANGULIZI.

Wakala wa Huduma za Misitu(TFS) Wilaya ya Wanging'ombe ina eneo la utendaji lenye ukubwa wa kilometa za mraba 3570.Katika eneo hilo kuna jumla ya misitu ya vijiji 31 yenye ukubwa wa hekta 5248.31ambayo ipo chini ya Ushirikishaji na utunzaji wa misitu ya vijiji (Participatory Forest Management).Wakala wa Huduma za Misitu Wilaya ya Wanging'ombe ina jumla ya watumishi watatu (3) ambao ni Mhifadhi Mkuu pamoja na wasaidizi wawili.

Ofisi kuu ya Wakala wa Huduma za Misitu Wilaya ya Wanging'ombe ipo Tarafa ya Mdandu Kata ya Igwachanya Kijiji cha Igwachanya kwenye jengo/ofisi ya TARURA, pia TFS -Wanging'ombe tuna ofisi ndogo iliyopo katika Tarafa ya Imalinyi Kata ya Makoga Kijiji cha Makoga.

B: KAZI ZILIZOFANYIKA NA OFISI YA WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU WILAYA YA WANGING'OMBE KWA KIPINDI CHA JULAI – MARCH 2021

Wakala wa Huduma za Misitu Wilaya ya Wanging'ombe imefanya kazi zifuatazo;-

(i) DORIA.

Kwa kipindi cha robo tatu ya mwaka tumefanya doria 17 ndani na nje ya misitu ya vijiji vya Saja, Mayale Uhenga, Igando, Mtapa,Iyayi,Uhenga na Luduga ili kuzuia shughuli za ukataji miti pamoja na uchomaji wa mkaa usiofuata kanuni na taratibu za misitu. Na katika doria hio tumebaini mapungufu ya ukatajwi ovyo wa misitu ya vijiji ambayo imehifadhiwa kisheria,na kukamata gunia za mikaa 180 zilizovunwa kinyume na sheria ya misitu Na 14 ya mwaka 2002.

(i) UTOAJI WA ELIMU.

Kwa kipindi cha robo tatu ya mwaka tumetoa elimu ya uhifadhi wa misitu na utaratibu wa usafirishaji wa mazao ya misitu na nyuki katika vijiji vya Mtapa,Itambo, Luduga, Hanjawanu na Mgate.Pia elimu itaendelea kutolewa kwa vijiji vingine vyenye misitu ya hifadhi, lengo ni kunusuru misitu hiyo na dhumuni ya elimu hio ni kujenga uelewa kwa wananchi kupata vibali vya uvunaji,usafirishaji, na uuzaji wa mazao ya misitu na nyuki.

(i) UKUSANYAJI WA MADUHURI.

Kwa kipindi cha robo tatu ya mwaka tumekusanya kiasi cha Tsh 63,327,914/= sawa na 101% *ya makusanyo kwa mwaka,ambazo zimetokana* na vyanzo mbalimbali ikiwemo Ushuru wa kuni, mkaa, utoaji wa vibali vya kusafirisha mazao ya misitu na nyuki (Transit Pass),pamoja na faini za makosa mbalimbali kulingana na sheria ya misitu ya mwaka 2002.

(i) UGAWAJI WA MICHE YA MITI.

Wakala wa Huduma za Misitu Wilaya ya Wanging'ombe imegawa miche ya miti 750 ya Syzigium Spp(mivengi) kwa ajili ya kupanda pembeoni mwa vyanzo vya maji ili kunusuru vyanzo hivyo visikauke na kuzuia mmonyoko wa udongo.Vyanzo vya maji vilivyo pandwa miche ya miti ni Chamfudu,Chelelo na Litundu vilivopo kijiji cha Luduga ambavyo vilipandwa miche 400 na miche 50 ilipandwa kijiji cha Liutundu Tarafa ya Wanging'ombe na miche 300 ilipandwa pembezoni mwa chazo cha mto chamavengi kilichopo kijiji cha Itambo tarafa Mdandu.

C: CHANGAMOTO.

Wakala wa Huduma za Misitu Wilaya ya Wanging'ombe inakumbwa na changamoto mbalimbali ikiwemo;-

i. Upungufu wa watumishi hususani askari wajeshi la uhifadhi kwaajili ya kazi za doria.
ii. Vitendea kazi kama gari kwaajili ya shughuli za doria na uelimishaji jamii juu ya uhifadhi wa misitu na mazingira kwa ujumla.
iii. Ukataji wa miti ya hifadhi hususani maeneo ya vijiji vya Saja, Uhenga na Igando.
iv. Utoaji wa vibali vya uvunaji na usafirishaji kwa watendaji wa serikali za vijiji bila kushirikisha ofisi ya TFS Wilaya ya Wanging'ombe

D: MKAKATI WA KUTATUA CHANGAMOTO.

Wakala wa Huduma za Misitu Wilaya ya Wanging'ombe imeomba kuletewa askari watatu(3) wa Jeshi la Uhifadhi na gari moja Toyota Land Cruiser(double cabin) kwaajili ya shughuli za doria kwenye misitu ya hifadhi na barabarani,na pia imejipanga kuongeza elimu ya uhifadhi kwenye vijiji vya Itambo, Luduga, Sakalenga, Uhenga, Iyayi, Igandon.kambavo ina misitu ya hifadhi na kugawa miche ya miti kwa taasisi za serikali na watu binafsi.

Naomba kkuwasilisha,

Abdu Heriel Mnjokava.
KNY; MHIFADHI MISITU(W).
WILAYA YA WANGING'OMBE